

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**15 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA – TAREHE 15 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

420. **MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO**  
**MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itanza kutekeleza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara ya Bomang'ombe – Rudugai – Chekimaji – Kikafu chini – Kawaya – Mijengweni – Shing'oro Mferejini hadi Mako.

421. **MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI**  
**MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa Kilomita tano ndani ya Mji wa Bagamoyo itatekelezwa.

**422. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na Kituo cha Afya kwa kila Kata ili kupunguza vifo vya Mama na Mtoto.

**WIZARA YA NISHATI:**

**423. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Mradi wa kusambaza umeme katika Jimbo la Kibaha Mjini unakwenda kwa kusuasua:-

Je, ni lini Mradi huo utakamilika ili Wananchi wa Kibaha Mjini waondokane na adha ya umeme.

**424. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi ya kufikisha Umeme wa Msongo mkubwa katika Mkoa wa Katavi.

**425. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Jimbo la Tunduru Kusini lina Vijiji 6 vyenye umeme kati ya 65:-

- (a) Je, ni lini Mradi wa REA awamu ya tatu utaanza;
- (b) Je, ni lini umeme wa ujazilizi wa maeneo ambayo hayana umeme hasa Vitongoji vya Vijiji vya Azimio, Chiwana, Umoja, Mkandu, Mbesa, Airport, Namasalau, Tuwemacho, Ligoma, Mchuruka na Makoteni vitapatiwa umeme.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**426. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

- (a) Je, ni lini Kata 16 zisizo na mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Urambo zitapatiwa mawasiliano na kuwaondolea Wananchi adha ya kukosa mawasiliano;

- (b) Je, ni kwa nini baadhi ya maeneo yana Minara ya simu lakini kuna matatizo ya mawasiliano.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **427. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Katesh – Haydom kwa kiwango cha lami ili kuwarahisishia Wananchi kupata huduma za

- afya katika Hospitali ya Haydom pamoja na usafirishaji wa mazao hasa ngano.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **428. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Makamu wa Rais ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Tarafa ya Simbo na Manonga katika Jimbo la Manonga.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **429. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

- (a) Je, ni lini Wananchi wa Ludewa ambao maeneo yao yamechukuliwa na Serikali kwa muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma watalipwa fidia;
- (b) Je, ni lini Mradi wa Liganga na Mchuchuma utanza kufanya kazi ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Njombe na Taifa kwa ujumla.

### **III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA**  
**15 JUNI, 2021**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**